

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Taarifa kwa Vyombo vya Habari kuhusu Kaya zilizoondolewa kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Katika Awamu ya Tatu ya TASAF

1. Utangulizi

Katika Awamu ya Tatu ya TASAF iliyoanza mwaka 2012 Serikali inatekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ambapo kaya milioni moja na laki moja na elfu kumi mia sita thelathini na tano (1,110,635) zimeandikishwa Katika Mpango huu. Kaya huandikishwa baada ya hatua ya utambuzi ambayo huhusisha jamii kufanya mikutano ya pamoja na kujiwekea vigezo vya umaskini na kutambua kaya maskini na baadaye kaya hizo kufanyiwa uhakiki kwa kutumia njia za kitakwimu na viashiria vya umaskini. Kwa kutambua kwamba Watanzania wenzetu takribani 28.2% bado ni maskini sana, Serikali imekusanya Mapato. Kaya maskini zilizoandikishwa hupokea ruzuku kila baada ya miezi miwili ili ziwekeze kwenye lishe, afya na elimu. Kadhalika Kaya hizo hulipwa ujira kwa kushiriki kwenye miradi ya kujiongezea kipato kwa mafano; ujenzi wa Barabara, marambo ya maji nk. kama mkakati endelevu ambao lengo lake ni kuondokana na umasikini na hivyo kuacha kutegemea ruzuku inayotolewa na Serikali kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini katika Awamu ya Tatu ya TASAF. Hadi sasa Serikali imeshatumia Shilingi 391,835,484,755 zilizolipwa katika mikupuo 8 kwa Kaya 1,110,635.

2. Maagizo ya Serikali kuhakiki kaya kwenye Mpango

Pamoja na lengo zuri la Mpango huu, hata hivyo ofisi yangu imepokea malalamiko mengi kwamba baadhi ya kaya zilizofaika hazistahili.

